

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA AFYA

Telegram "AFYA", **DODOMA**  
Namba ya Simu: +255 26 2323267  
Nukushi No: +255 22 2138060  
Barua zote zitumwe kwa **Katibu Mkuu**



Mji wa Serikali – Mtumba,  
Barabara ya Afya,  
S.L.P 743  
**40478, DODOMA**

**16 Januari, 2024,**  
**Dodoma.**

### TAARIFA KWA UMMA

#### **KUHUSU KUFUTWA KWA MATOKEO YA MTIHANI WA USAJILI NA LESENI YA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA KWA WATAHINIWA 1,330 WA STASHAHADA**

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Wizara ya Afya lina jukumu la kusimamia taaluma za Wauguzi na Wakunga nchini kupitia Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010. Pamoja na majukumu mengine ya msingi, Baraza limepewa jukumu la kusajili, kuorodhesha, na kutoa leseni kwa wauguzi na wakunga wa ngazi zote, kwa kuendesha Mitihani ya Usajili na Leseni kwa Mujibu wa Kifungu cha 15(a) (b) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010.

Mnamo tarehe 07/09/2023, Baraza liliendesha mitihani ya usajili na leseni kwa Wauguzi na Wakunga 1,434 wa ngazi zote. Watahiniwa wa Astashahada walikuwa 44, Stashahada 1,330, Shahada 60. Mitihani hii ilifanyika katika vituo vitatu katika Mikoa ya Dar Es Salaam (DUCE); Mwanza (Mwanza University) pamoja na Dodoma (St. John University)

Wizara ya Afya ilipata taarifa za kuvuja kwa mtihani na kuchukua hatua za haraka kushirikiana na Vyombo vya Usalama kufanya uchunguzi ambapo ilithibitika kuwa ni ukweli mtihani ulivuja na kusambaa kwa watahiniwa wa Stashahada. Mtuhumiwa aliyehusika katika uvujishaji wa mtihani huu tayari amebainika na kusimamishwa kazi huku taratibu kinidhamu na kisheria zinaendelea kutekelezwa.

**Wizara inautangazia umma kuwa matokeo yote ya mtihani wa usajili na leseni wa Wauguzi na Wakunga kwa watahiniwa wa Stashahada yamefutwa kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010, Kanuni ya mafunzo ya Mwaka 2010, Kifungu cha 22(3)**

Hatua hizi zimechukuliwa kwa lengo la kuhakikisha Baraza linathibitisha wataalam wenye sifa stahiki kulingana na taaluma zao kutoa huduma bora za matibabu kwa wagonjwa pamoja na kuzingatia usalama wa mteja anayetegemea kupata huduma za Uuguzi na Ukunga. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010, ambalo ndilo jukumu kubwa la Baraza.

**Watahiniwa watapewa nafasi ya kufanya mtihani mwingine bila malipo yoyote na hawatahitajika kujisajili tena, mtihani utafanyika tarehe 16/02/2024, Dodoma.** Taarifa zaidi kuhusu kurudia kwa mtihani huu zitatolewa na Baraza hivyo watahiniwa wote wanatakiwa kujiandaa na mtihani huo kwa kufuata taratibu kanuni na sheria.

Kwa upande wa watahiniwa wa ngazi za Astashahada na Shahada matokeo tayari yameshatoka na watahiniwa wamepata matokeo yao.

Imetolewa na:-

  
Englibert Kayombo

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA  
MAWASILIANO SERIKALINI**